FUNZO LA 52

1. Nikodemo alijuaje kwamba Mungu alimtuma Yesu?
-Kwa sababu Yesu alikuwa akifanya miujiza mingi ambayo ni Mungu tu ndiye aliyeweza kufanya.

2. Je, "kuzaliwa kwa maji" kunamaanisha "kubatizwa"?
-La.

3. Je, ubatizo unaweza kutuokoa?
-La.

4. Yesu alimaanisha nini "kuzaliwa kwa maji"?
-Kuzaliwa kwa maji inamaanisha kwamba lazima tutubu dhambi zetu ili Mungu atusafishe dhambi zetu.

5. Yesu alimaanisha nini "kuzaliwa kwa Roho"?
-Kuzaliwa kwa Roho inamaanisha kwamba Mungu Roho Mtakatifu lazima atoe maisha mapya kwa roho zetu.

6. Yesu alimaanisha nini, "Mwili huzaa mwili, lakini Roho huzaa roho?
-Yesu alikuwa na maana kwamba mwili unaweza kuzaa tu mwili.
-Yesu pia alimaanisha kwamba Mungu Roho Mtakatifu ndiye pekee anayeweza kuzaa roho ya mwanadamu.

7. Kwa mujibu wa Mungu, ni watu aina gani mbili tu duniani?
-Wale ambao wamezaliwa mara moja tu, na wale ambao wamezaliwa mara ya pili.



8. Je, watu ambao wamezaliwa mara moja tu wako katika familia ya nani ?
-Wapo katika familia ya Shetani.

9. Je, watu ambao wamezaliwa mara ya pili wako katika familia ya nani ?
-Wapo katika familia ya Mungu.

10. Ni vipi Yesu na yule nyoka wa shaba ambaye Mungu alimwamuru Musa afanye jangwani wanafanana?
-Kama vile nyoka wa shaba alikuwa ametundikwa juu ya mti, ndivyo Yesu pia angetundikwa juu.
-Kama vile Waisraeli waliokolewa walipomtazama yule nyoka wa shaba, ndivyo Yesu pia angewaokoa wale wanaomwamini.

11. Kwa nini Mungu alimtuma Yesu katika ulimwengu huu?
-Mungu alimtuma Yesu kutuokoa kutoka kwa nguvu ya dhambi, mauti, na Shetani.

12. Je, wale wanaomwamini Yesu watahukumiwa na Mungu?
-La.

13. Kwa nini wale ambao hawamwamini Yesu tayari wamehukumiwa na Mungu?
-Kwa sababu hawaamini kwamba Yesu ni Mungu Mwokozi.

14. Kwa nini watu hawataki kusikiliza Neno la Mungu?
-Kwa sababu wanapenda dhambi zao.

-Siku moja, Yesu alirudi katika kijiji cha Kapernaumu.

Tusome Marko 2:1-2

1-Akaingia Kapernaumu tena, baada ya siku kadha wa kadha, ikasikiwa ya kwamba yumo nyumbani.
2-Wakakusanyika watu wengi, isibaki nafasi hata mlangoni; akawa akisema nao neno lake.

-Watu wengi walikuja kumsikia Yesu akifundisha.
-Yesu aliwafundisha Neno la Mungu.

-Neno la Mungu ambalo Yesu alifundisha ni Neno lile lile la Mungu ambalo tunakufundisha hivi sasa.

-Neno la Mungu halibadiliki.
-Neno la Mungu ni sawa kwa watu wote.

-Kama vile watu walimsikiliza Yesu akifundisha Neno la Mungu, Mungu anataka usikilize tunapokufundisha Neno la Mungu.

-Kwa sababu Yesu alikuwa akifundisha ndani ya nyumba, na watu wengi walikuwa wamekuja kumsikia Yesu akifundisha, hakukuwa na nafasi tena ndani ya nyumba hiyo.

-Hata nje ya mlango, hakukuwa na nafasi tena.

-Yesu alipokuwa akifundisha, watu wengine walimletea mtu aliyepooza.

Tusome Marko 2:3



3-Wakaja watu wakimletea mtu mwenye kupooza, anachukuliwa na watu wanne.

-Mtu aliyepooza aliweza kujiponya?
-La.

-Je, marafiki wa yule aliyepooza waliweza kumponya?
-La.

-Je, kuna daktari yeyote aliyeweza kumponya yule aliyepooza?
-La.

-Kama vile mtu huyu aliyepooza hakuweza kujiponya, hakuna mtu anayeweza kujiokoa kutoka kwa nguvu ya dhambi, kifo, na Shetani.

-Je, wanaume walifanya nini na yule mtu aliyepooza?

Tusome Marko 2:4

4-Na walipokuwa hawawezi kumkaribia kwa sababu ya makutano, waliitoboa dari pale alipokuwapo; na wakiisha kuivunja wakalitelemsha godoro alilolilalia yule mwenye kupooza.

-Kwa sababu kulikuwa na watu wengi wakimsikiliza Yesu akifundisha, na hakukuwa na nafasi tena ndani ya nyumba, wale watu walimpeleka yule mtu aliyepooza juu ya paa la nyumba.

-Walivunja shimo kupitia paa la nyumba, na kumshusha yule mtu aliyepooza chini kwenye mkeka wake wa kulala mbele ya Yesu.

-Kwa sababu Wayahudi walijenga nyumba zao na paa tambarare zilizotengenezwa kwa tope na majani, wanaume hao waliweza kuvunja shimo kupitia paa, na kumshusha yule mtu aliyepooza mbele ya Yesu.

-Je, wanaume walimleta kwa nani mtu aliyepooza?
-Kwa Yesu.

-Ni nani pekee aliyeweza kumponya yule aliyepooza?
-Yesu.

-Yesu alifanya nini?

Tusome Marko 2:5

5-Naye Yesu, alipoiona imani yao, akamwambia yule mwenye kupooza, Mwanangu, umesamehewa dhambi zako.

-Yesu aliona kwamba wale wanaume walimwamini kweli, na alimsamehe yule aliyepooza dhambi zake.

-Kulikuwa na waalimu wa sheria ambao walikuwa wamekaa ndani ya nyumba hiyo.

-Yesu alipomsamehe yule mtu aliyepooza dhambi zake, hawa waalimu wa sheria walifikiria nini?



Tusome Marko 2:6-7

6-Na baadhi ya waandishi walikuwako huko, wameketi, wakifikiri mioyoni mwao,
7-Mbona huyu anasema hivi? Anakufuru. Ni nani awezaye kusamehe dhambi isipokuwa mmoja, ndiye Mungu?

-Walimu wa sheria walikuwa wakifikiria kwamba ni Mungu tu anayeweza kusamehe dhambi.

-Je, Walimu wa sheria walikuwa wanafikiria vizuri?
-Ndiyo.

-Ni kweli kwamba ni Mungu tu anayeweza kusamehe dhambi?
-Ndiyo.

-Je, kuna mtu yeyote anayeweza kusamehe dhambi?
-La.

-Je, kuhani anaweza kusamehe dhambi?
-La.

-Kwa nini Yesu aliweza kuwasamehe watu dhambi zao?
-Kwa sababu Yesu ni Mungu.

-Walimu wa sheria pia walikuwa wakifikiria kwamba Yesu alikuwa akimkufuru Mungu.

Je, walimu wa sheria walikuwa wanafikiria vizuri?
-La.

-Ni kweli kwamba Yesu alikuwa akimkufuru Mungu?
-Hapana.

-Yesu hakuwa akimkufuru Mungu.

-Je, Yesu alijua kile walimu wa sheria walikuwa wanawaza?

Tusome Marko 2:8

8-Mara Yesu akafahamu rohoni mwake kwamba wanafikiri hivyo nafsini mwao, akawaambia, Mbona mnafikiri hivi mioyoni mwenu?

-Japokuwa waandishi wa sheria hawakusema chochote, Yesu alijua wanachofikiria.

-Kwa sababu Yesu ni Mungu, alijua mawazo yote ya watu wote.

-Kisha, Yesu alisema nini?

Tusome Marko 2:9-12

9-Vyepesi ni vipi, kumwambia mwenye kupooza, Umesamehewa dhambi zako, au kusema, Ondoka, ujitwike godoro lako, uende?
10-Lakini mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi, (hapo amwambia yule mwenye kupooza),
11-Nakuambia, Ondoka, ujitwike godoro lako uende



nyumbani kwako.
12-Mara akaondoka, akajitwika godoro lake, akatoka mbele yao wote; hata wakastaajabu wote, wakamtukuza Mungu, wakisema, Namna hii hatujapata kuiona kamwe.

-Yesu aliwaambia watu kwamba alikuwa na mamlaka ya kusamehe dhambi.

-Kwa nini Yesu alikuwa na mamlaka ya kusamehe dhambi?
-Kwa sababu Yesu ni Mungu.

-Yesu alionyesha nguvu zake kama Mungu kwa kumponya kabisa mtu aliyepooza.

-Kwa nini Yesu aliweza kuponya wagonjwa?
-Kwa sababu Yesu ni Mungu.

-Ni Mungu tu ndiye aliyeweza kumponya yule aliyepooza.

-Baada ya hapo, Yesu alitoka akaenda ziwani karibu na kijiji cha Kapernaumu.

Tusome Marko 2:13-14

13-Akatoka tena, akaenda kando ya bahari, mkutano wote ukamwendea, akawafundisha.
14-Hata alipokuwa akipita, akamwona Lawi wa Alfayo, ameketi forodhani, akamwambia, Nifuate. Akaondoka akamfuata.

-Yesu alipokuwa anatembea, alikutana na mtu aliyeitwa Lawi.

-Jina la pili la Lawi lilikuwa lipi?
-Mathayo.

-Ni kazi gani Mathayo alifanya wakati Yesu alimwita?
-Mathayo alikuwa mtoza ushuru.

-Mathayo alikusanya ushuru kwa niaba ya Warumi, akichukua ushuru kutoka kwa watu wake, Wayahudi.

-Kwa sababu watoza ushuru walichukua ushuru kutoka kwa watu wao wenyewe, na kuwapa Warumi, Wayahudi waliwachukia.

-Wayahudi pia walichukia watoza ushuru kwa sababu watoza ushuru walikuwa wabaya sana.

-Wakusanya ushuru waliwalazimisha Wayahudi kulipa ushuru zaidi, ambao watoza ushuru walijiwekea.

-Yesu alimwita Mathayo mtoza ushuru amfuate.
-Kwa nini Yesu alimwita mtoza ushuru amfuate?

-Kwa sababu Mathayo alielewa kuwa alikuwa amemkosea Mungu.

-Kwa sababu Mathayo alielewa kuwa Mungu huadhibu dhambi zote kwa kifo.



-Kwa sababu Mathayo alielewa kuwa ni Mungu tu ndiye aliyeweza kumwokoa.

-Kwa sababu Mathayo alielewa kuwa Yesu alikuwa Mwokozi.

-Miaka mingi baadaye, Mungu Roho Mtakatifu alimwongoza Mathayo kuandika moja ya vitabu katika Biblia ya Mungu.

-Kwa sababu Mathayo alifurahi kumwamini Yesu kama Mwokozi wake, Mathayo alimwalika Yesu na watu wengine nyumbani kwake kula.

Tusome Marko 2:15-16

15-Hata alipokuwa ameketi chakulani nyumbani mwake, watoza ushuru wengi na wenye dhambi waliketi pamoja na Yesu na wanafunzi wake; kwa maana walikuwa wengi wakimfuata.

16-Na waandishi na Mafarisayo walipomwona anakula pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi, waliwaambia wanafunzi wake, Mbona anakula pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi?

-Walimu wa sheria ambao walikuwa Mafarisayo walisema nini walipomwona Yesu akila na Mathayo na watu wengine?

-Walisema, “Kwa nini Yesu anakula pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi?”

-Mafarisayo hawakuamini kuwa wao ni wenye dhambi.

-Mafarisayo waliamini kwamba hawakuwa na dhambi.

-Mafarisayo hawakuelewa kuwa watu wote wamezaliwa katika dhambi.

-Mafarisayo hawakuelewa kuwa watu wote wamemkosea Mungu.

-Yesu alisema nini aliposikia yale Mafarisayo walisema?

Tusome Marko 2:17

17-Yesu aliposikia aliwaambia, Wenye afya hawahitaji tabibu, bali walio hawawezi; sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi.

-Yesu aliwaambia Mafarisayo kuwa watu wenye afya hawahitaji daktari, lakini wagonjwa wanahitaji.

-Yesu alimaanisha nini?

-Yesu alimaanisha kwamba hakuja kuwaokoa watu ambao hawajui kuwa wao ni wagonjwa.

-Yesu alikuja kuokoa watu tu ambao wanajua kuwa wao ni wagonjwa.

-Ufuatao ni mfano:

-Ikiwa mtu ni mgonjwa lakini hajui, je, huenda kwa daktari?



-La.

-Kwa nini mgonjwa haendi kwa daktari?
-Kwa sababu hajui kuwa anaumwa.

-Yesu hakuja kuokoa watu ambao wanaamini kuwa hawana dhambi.

-Ni nani ambaye Yesu alikuja kuokoa?

-Yesu alikuja kuokoa watu tu ambao wanajua kuwa wamemkosea Mungu, na kwamba ni Mungu tu ndiye anayeweza kuwaokoa.

-Na wewe je?

-Unajua kuwa ulizaliwa katika dhambi?
-Je, unajua kuwa umemkosea Mungu?

-Unajua kwamba Mungu huadhibu dhambi zote na kifo cha milele?

-Unajua kuwa ni Mungu Mwokozi tu ndiye anayeweza kukuokoa?

-Ikiwa unajua hii, basi Yesu alisema kwamba alikuja ulimwenguni kuwa Mwokozi wako.